

## Zaidi ya watoto milioni mbili wapo katika ajira mbaya nchini

Na Sharifa Marira

ZAJIDI ya watoto ya milioni mbili wako katika ajira mbaya nchini, hali inayosababishwa na wazazi au walezi kushindwa kutoa ushirikano kwa serikali katika kukemea watu wanaowatumikisha badala yake wanashirikiana nao.

Hayo yamesemwa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Kazi na Ajira, Gaudencia Kabaka, wakati wa uzinduzi wa mpango wa kuzuia utumikishwaji wa watoto katika mashamba ya tumbaku (Prosper).

"Wazazi wengine unakuta wanashirikiana na watu hawa kuwafikisha watoto kwenye ajira mbaya, hata kama maisha ni magumu hamuoni kuwa mahatarisha maisha ya watoto?" alihoji na kuongeza: "Naombeni tushirikiane katika kukomesha tatizo hili."

Akizungumzia mpango wa Prosper, alisema mradi huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kukomesha ajira mbaya kwa watoto na kutoa elimu kwa jamii na utaelekeza nguvu zaidi katika wilaya za Urambo na Sikonge mkaoni Tabora.

Alifanua kuwa mtoto mwenye umri wa chini ya miaka 14 hatakiwi kujiriwa, na sheria iko wazi kuwa atakayemuajiri mtoto aliye chini na umri huo atatozwa fami isiyozidi Sh. milioni tano.

Aidha, alieleza kuwa kuanzia Julai 2011 hadi Disemba 2015, watoto 6,000 walio na umri kati ya miaka mitano hadi 17, wataondolewa katika ajira mbaya na watoto 1,800 wenye umri kati ya miaka mitano hadi 17 watazuiliwa kujiunga na ajira mbaya.

PICHA NA MPIGA PICHA WETU



Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Gaudencia Kabaka (kushoto), akinyanyua juu waraka maalum baada ya kuzindua mradi wa kutokomeza ajira kwa watoto katika mashamba ya tumbaku (ECLT). Anayeshuhudia ni Makamu wa Rais wa ECLT, ambayo pia ni asasi ishiyo ya kiserikali yenye makuu yake Geneva, Uswisi Iktwa Imeanzishwa na wadau wa tumbaku duniani kusatidia juhudi za kutokomeza ajira kwa watoto katika sekta hiyo.